# *MMOJA KATIKA MILIONI MOJA*

Asante, Ndugu Shakarian. Na habari za asubuhi, marafiki. Kwa kweli ninafurahi kuwa hapa Los Angeles tena asubuhi ya leo, kabla ya mkutano huu mkuu, na mkutano ujao wa juma hili lijalo kule kwenye Hoteli ya Embassy. Ninatarajia kuwaona ninyi nyote kule. Na sisi sote tuna matarajio makubwa ya kukutana na Bwana wetu Yesu, kumwona Yeye kule. Aliahidi ya kwamba atakuwa huko. "Palipo wawili ama watatu waliokusanyika pamoja," Yeye angekuwako hapo.

2 Na nina hakika ya kwamba nilikutana Naye asubuhi ya leo nilipokuwa ninapanda vipandio hapa katika ukumbi huu wa mikutano, wakati ambapo watu wote walikuwa na matarajio makubwa, wakingojea kiamshakinywa na mahubiri. Na ni vyema kukusanyika hapa pamoja nanyi, na kwa wanaosikiliza redio. Kuna watu wengi sana hapa ndani, waninii...ilibidi nishuke niende kwenye orofa ya pili, na nikawazungumzie wachache. Na nimeona maombi mengi sana, matatizo ya moyo, na maradhi mbalimbali ya miili yao, nasi tuko hapa sasa kuwaombea wagonjwa na wanaoteseka.

3 Mara nilipofika mwisho wa vipandio...Ninamwangalia yule mzee muungwana sasa. Alinijia, na kusema, "Ndugu Branham, miaka mingi iliyopita..." Alisema aliumwa sana na ugonjwa wa moyo hata a-...walifikiri atakufa. Nami nilimwombea, ndipo neema ya Mungu ikamponya. Naye huyu hapa asubuhi ya leo, kwenye umri uliozidi sana miaka themanini, akishangilia tu. Kwa hiyo hilo linatufanya tushikilie zaidi.

4 Na sasa bila shaka ninahitaji sana maombi ya watu wanaosikiliza redio, na walio hapa pia. Nikiisha kuondoka kwenye mkutano huu, ninaenda Ulaya, nishuke kwenda Afrika na ko kote kule, kwa ajili ya mikutano. Na hii ni kwenda kwa ono, kwa hiyo utakuwa ni mkutano mkubwa kule, nina hakika. Na nilijisikia kwa muda mrefu ya kwamba Bwana amenitaka nirudi. Huduma nyenyekevu, huduma ndogo ambayo Yeye alinipa, sidhani tayari ameisha maliza nayo kabisa, kule. Inaonekana kana kwamba huenda kukawa na mtu mahali fulani ningeweza kumshika katika jarife la Injili, ile ambayo amenipa kuvua nayo watu, kwa njia ya uponyaji wa Kiungu, kuwaombea wagonjwa. Na kwa kweli ninatamani maombi yenu, ninyi watu hapa na hao huko nje wanaosikiliza redio.

5 Sasa sina wakati ni kuchukua tu somo na kuhubiri, jambo ambalo ninalitarajia baada ya dakika chache hapa kwenye ninii—kwenye...ukumbi huu wa mikutano, bali ni kuzungumza tu na—nanyi dakika chache, tupate kufahamiana. Na kwa

watu walioko huko nchini, nitaomba maombi kwa ajili ya hao walio huko nje, mara moja, na hapa ndani pia. Nami kwa kweli ninafurahia kukutana na marafiki wote hawa wazuri waliongezeka wapya ambao sijawahi kukutana nao, nimekutana nao tu asubuhi ya leo.

6 Tumekuwa na wakati mzuri sana kwenye ibada mahali pengine. Sitokitoki sana tena, kuna kazi nyingi sana. Tunajaribu tu kuifanya barabara iwe moto kati ya Jeffersonville, Indiana na Tucson, Arizona, ambako tulihamia miaka michache iliyopita, kwa ono la Bwana, lililotutuma kule, pia, bila kujua nilikokuwa ninaenda. Na wengi wenu hapa, hapa Clifton, nilizungumza nanyi muda kidogo kabla sijaondoka kwenye mkutano wa Phoenix, juu ya ono lililokuwa limetokea. Niliona malaika saba katika kundi.

7 Na ninajua, kwa wanaosilikiza redio, labda wengi wenu si wa Injili yote, na jambo hili linaweza kuonekana kidogo ni la ajabu kwenu. Ambapo, lingekuwa hivyo kwangu, bali kuna . . . Mtu ye yote anayeweza kuelezea jambo lo lote, huna haja tena kulikubali kwa imani. Ni mambo tusiyoweza kuelezea, ndiyo tunayopaswa kuyakubali kwa imani. Hatuwezi kumwelezea Mungu. Hakuna mtu anayeweza kumwelezea Mungu. Yeye ni mwenye enzi, Naye ni mkuu na mwenye nguvu. Tunaninii tu—tunalikubali tu kwa maana kwamba tunajua Yeye yuko. Na basi kwa imani yetu, katika kukubali jambo hilo, Yeye anatuletea jibu, ule ubatizo wa Roho Mtakatifu.

8 Ambalo, nitawazungumzia tu juu ya jambo hilo, katika dakika chache hapa, juu ya, "Njia ya Mungu, mahali pa kuabudia." Na mahali pekee unapoweza kumwabudu, mahali pekee atakapowahi kukutana nawe, inabidi kuwe . . . Kuna kanisa moja, mahali pamoja, wakati mmoja, kundi moja la watu, katika wote ambao Mungu anakutana nao. Nami ninatumaini ya kwamba Bwana ataubariki Ujumbe huo kwenye mioyo yenu hapa.

9 Sasa, nilipokuwa nikija Tucson, ilikuwa ni ajabu, maono hayo yakinena nanyi katika Jina la Bwana. Hakuna hata moja la hayo kadiri ninavyoweza kukumbuka, nitamwuliza mtu mwingine ye yote kama wanaweza kukumbuka wakati wo wote, ambapo Yeye alipata kusema jambo lo lote ila lililokuwa ni Kweli. Sikuzote linatukia vile vile tu Yesu anavyosema litatukia.

10 Naye anapaswa kuninii, kulingana na Maandiko, kurudi kwetu katika siku hizi za mwisho, katika huduma ya namna hii. Hiyo itakuwa ni baada ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kunena kwa lugha, na uponyaji wa Kiungu, na kadhalika, mambo haya. Kule kufikia kilele cha ujumbe wa kipentekoste ndiko tunakozungumzia leo. Hii huduma ya Kristo Mwenyewe akifanyika mwili katika watu Wake, wakiwa na mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani; katika Mwili Wake,

Bibi-arusi, ambaye ni sehemu Yake, akifanya mambo yale yale, kama Mume na Mke, ama Mfalme na Malkia, kabla tu ya sherehe ya Arusi.

11 Juma hili, Bwana akipenda, ninataka kuzungumzia baadhi ya mambo hayo, huko kwenye mkutano wetu hapa, kwenye Ho—Hoteli ya Embassy, na kwa namna fulani mpate kulitambua jambo hilo katika njia yangu nyenyekevu ya kufanya hivyo. Wa—wakati na saa tunayoishi, kama mtu hajui aendee njia gani, afanye nini au aelekee wapi, wewe hu—huenendi kwa imani tena; unakisia tu, unathubutu tu. Na *kuthubutu* ni "ku—kuendea jambo bila ruhusa ya rasmi." Kwa hiyo kama hatuna ruhusa halisi rasmi kujua yale Mungu aliyosema yatatukia katika saa hii, tutaukabilije wakati huu? Nasi hatuna budi kukabiliana nao, tukijua, kwa imani katika Neno Lake, mambo yale yanayopaswa kuwa yanatendeka sasa; na hali ya mataifa, hali ya watu, hali ya kanisa, na kadhalika.

12 Hatuna budi kujua hayo, na halafu jinsi ya kutoka kwenda kuyakabili hayo. Kama hujui jinsi ya kulifanya jambo hilo, wewe ni ninii tu—kile tu tulichokuwa tukiita, kwa namna fulani, shaghlabaghla; unalirukia tu, ukitumainia litakuwa hapa, ukitarajia *hiki* na kutarajia *kile*, na "je! litatukia?" Lakini Mungu hataki sisi tufanye hivyo. Anataka tujue yale aliyosema kuhusu siku hii ya leo, na ndipo tukabiliane nayo kwa imani, kwa maana Yeye alisema itakuwa hivyo. Ndipo sisi—tunajua wewe ni Kweli basi, kwa maana huchukui neno la mtu fulani kwa jambo hilo; umeshikilia Neno Lake kuhusu yale tunayopaswa kufanya. Nasi tunatarajia ya kwamba Baba yetu wa Mbinguni ata—atatujalia jambo hili juma hili.

13 Sasa, ninasikitika ya kwamba nilikatiza, yale niliyokuwa nikisema dakika chache zilizopita, kuhusu kuja Tucson. Nami nilifikiri, mimi mwenyewe, ya kwamba ilikuwa ndio mwisho wa maisha yangu. Nilifikiri kwamba hakuna mtu angaliweza kustahimili mshindo huo wa hali hiyo ilivyotukia katika ono hilo asubuhi hiyo, kwenye saa nne kule nyumbani, ambaye angeweza kuishi baada ya huo. Mbona, nilikuja Tucson, nikifanya matayarisho na mwanangu, kwa ajili ya mke wangu na—na watoto waende wakaishi pamoja naye baada ya mimi kuondoka, kwa sababu nilifikiri ulikuwa ndio mwisho wangu. Na mimi, huko Phoenix, ninyi watu mliokuwamo kwenye ile mikutano kabla halijatukia, niliwaambia jinsi tu lingetukia.

14 Vema, miezi michache baadaye, nilikuwa juu kwenye Magenge ya Sabino asubuhi moja, ambayo yako kaskazini tu mwa Tucson. Nilikuwa juu kule kuomba. Na nilipokuwa nikiomba, nilikuwa nimeinua mkono wangu hewani, nikisema, "Baba, ninakuomba ya kwamba Wewe kwa njia fulani utanisadia, nipe nguvu, kwa ajili ya saa ninayoikabili sasa. Na endapo kazi yangu imekwisha hapa duniani, basi sina budi kuja Kwako. Na si kwamba ninajutia kuja, bali ninajua ya kwamba

utaitunza familia yangu. Nami ni—ninaomba tu nipate nguvu kwa ajili ya saa hii." Ndipo kitu fulani kikaangukia mkononi mwangu!

15 Sasa, enyi wasikilizaji wa redio, hili nililosema linaweza kuonekana ni la kigeni, bali ni kweli. Na Mungu ndiye Hakimu wangu.

16 Nikaangalia kwenye mkono wangu, na ulikuwa umeshika upanga, wenye ala kwenye sehemu ya mpini. Na mpini wenyewe ulikuwa wa lulu, na ulionekana kama kinga ya dhahabu kwenye sehemu ya mpini. Na ki—kisu chenyewe kilionekana kana kwamba kwa namna fulani ulikuwa unang'ara, loo, kitu kama kromu ama cho chote kile kinachomeremeta juani.

17 Sasa, ilikuwa kama saa nne ama saa tano asubuhi, huko juu kabisa mlimani. Unaweza kuwazia jinsi mtu (ambapo ninajisikia kwamba niko na akili timamu) angejisikia akisimama pale akiwa na upanga asiojua ulikotoka, hakuna watu kwa maili na maili, ukiwa umeushika huo mkononi mwako. Niliuhisi, nikashika na kuutikisa ubapa wake huku na kule, na, mbona, ulikuwa ni upanga.

18 Ndipo nikaangalia kila upande. Nikasema, "Vema, sasa, jambo hilo lingepataje kutukia? Mimi huyu hapa nimesimama, papa, hapa, na hakuna mtu karibu kwa maili kadha wa kadha, basi huo ulitoka wapi?" Ndipo nikasema, "Vema, na—nadhani labda ni—ni Bwana akiniambia kwamba ni wakati wangu wa mwisho."

Ndipo Sauti ikanena ikasema, "Huu ni ule Upanga wa Bwana."

19 Basi nikawazia, "Sawa, upanga, basi ni kama ni wa mfalme, kumpandisha shujaa cheo." Unajua, jinsi ilivyokuwa huko Uingereza na kwenye nchi mbalimbali. Nikawazia, "Hiyo ndiyo kazi yake, kumpandisha shujaa cheo." Basi nikafikiri, "Vema, labda ninapaswa kuwawekea watu mikono, ama . . . " Nilikuwa na kila namna . . . Akili ya binadamu inaweza kuvurugikiwa kabisa, unajua. Hujui. Akili zetu zina kikomo; Yake haina kikomo. Kwa hiyo, na kama nilivyokuwa, u-. . . Ndipo ukaondoka mkononi mwangu wala sikujua ulikokwenda, ulitoweka tu. Mbona, kama mtu amekosa fahamu kidogo kuhusu mambo ya kiroho, u—ungeingia kichaa namna hiyo. Ungekuwa umesimama pale, ukishangaa ni nini kimetukia.

20 Ndipo Yeye akasema, "Ono hilo sio wakati wako wa mwisho. Ni kwa ajili ya huduma yako. Upanga huo ni Neno. Mihuri Saba itafunguliwa, siri zake . . . "

21 Na baadaye majuma mawili baada ya tukio hilo, ama miezi miwili, hasa, baada ya hilo, nilikuwa juu mlimani pamoja na kundi la marafiki wakati hilo, lilipotukia. Malaika Saba, dhahiri tu kama mtu unavyosimama hapa, walishuka kasi kutoka Mbinguni. Miamba milimani iliporomoka na kubingirika

chini ya vilima, na—na watu waliokuwa wamesimama pale walikuwa wanapiga mayowe na kupiga makelele, unajua, na vumbi likitimka kila mahali. Na hilo lilipotukia, Yeye akasema, "Rudi nyumbani kwako. Sasa itakuwa, kila Malaika atakuwa ni mmoja wa ile mihuri ya ile Mihuri Saba."

22 Ambapo, liko kwenye kanda. Na kitabu kinachohusu hayo kitatolewa hivi karibuni sana, kwa kuwa sasa kwa namna fulani kinawekwa katika lugha sanifu. Kama mjuavyo, sarufi yangu si nzuri sana, na watu wasingeninii. . .Itabidi tu mwe ni watu wanaonipenda na wajuao jinsi ya kunifahamu kwa sarufi yangu. Lakini mwanatheolojia fulani anakiweka katika lugha sanifu kwa niaba yangu, na kutoa ninii zote— ninii. . . Vema, labda nilitamka neno baya pale. Hata sijui. Kwa hiyo, nilimsikia mtu fulani akicheka, kwa hiyo nadhani ya kwamba hilo "kuweka katika lugha sanifu" haikuwa ni sawa. Lakini kama yule Mholanzi, nichukulieni kwa yale ninayomaanisha wala si yale ninayosema, kwa kweli.

23 Na ni dakika tatu tu sasa, ninaambiwa, kufikia wakati wa kufunga kipindi hiki.

24 Sasa, ninyi watu wapenzi mnaosikiliza redio, na nanyi mlio wagonjwa na wahitaji hapa mkutanoni, tafadhalini wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi sasa wakati tunapofanya maombi haya kwa ajili ya wagonjwa. Sasa, Yesu alisema, agizo Lake la mwisho kwa Kanisa, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." "Hao," hao waaminio! "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

25 Baba mpenzi wa Mbinguni, sisi ni kama watoto leo, tunatii yale Wewe uliyosema tufanye. Tunaweka mikono juu ya mahitaji haya yote kwa njia ya simu. Wewe unawaona huko kote nchini, jinsi walivyo wahitaji, hayo mateso. Unawaona wale hapa walio na haja, wanaoteseka. Nasi tunawakabidhi Kwako, Mungu Mpenzi, pamoja na imani hii katika Neno Lako ambalo Wewe umesema, "Ishara hizi zitafuatano na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Tujalie, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

[Ndugu Branham anamaliza matangazo ya kwanza ya redio—Mh.]

☆ ☆ ☆ ☆ ☆ ☆ ☆

26 Asante, Ndugu Shakarian. Bila shaka ni majaliwa makuu kurudi tena kwenye matangazo ya redio, kuzungumza na baadhi ya marafiki zetu huko nchini wanaosikiliza redio, pamoja na wale walioko hapa.

27 Na bila shaka tunawapa mwaliko huu, wa kuja kwenye Hoteli ya Embassy kesho alasiri, mpate kuombewa. Na si hivyo tu, bali waleteni hao wenye dhambi na hao waliorudi nyuma. Kama tukiwaombea wagonjwa peke yao, na tunamwona Mungu

daima akifanya miujiza mikuu, bali hilo ni la baadaye. Jambo muhimu ni kuokolewa, kujazwa na Roho wa Mungu, jambo ambalo nitazungumza nanyi katika muda wa dakika chache tu hapa, na utoshelevu jinsi ambavyo inatubidi kujazwa na Roho Mtakatifu.

28 Na uponyaji wa Kiungu kwa kawaida huuvuta usikivu wa watu, na huwaingiza katika Uwepo wa Mungu. Wakati Mungu anapofanya jambo fulani ambalo—ambalo wao wanajua halininii . . . vema, halieleweki. Hatuwezi kulionyesha kwa njia ya maumbile ya kawaida jinsi inavyotendeka. Mungu hulifanya jambo hilo kwa Njia Yake Mwenyewe iliyo kuu. Ndipo jambo hilo linavutia usikivu wa watu, kujua ya kwamba kuna Uwepo wa Nguvu fulani mahali fulani, ambao unaweza kufanya jambo fulani ambalo limepita ufahamu wa mwanadamu, na hilo linawafanya kumwangalia Mwana-Kondoo wa Mungu. Na daima, uponyaji wa Kiungu; nimeambiwa, nami ninaamini, mimi mwenyewe, ya kwamba kati ya asilimia sitini, labda, na sabini, ya huduma ya Bwana wetu, ilikuwa ni juu ya uponyaji wa Kiungu. Naye alifanya jambo hilo kuwavuta watu. Ndipo wakati walipokuwa hapo, Yeye alisema, "Msipoamini ya kwamba Mimi Ndiye, mtaangamia katika dhambi yenu."

29 Sasa, uponyaji wa Kiungu ni jambo kubwa la kuvutia, kuwafanya watu wamwangalie Bwana Yesu. Na Daktari F. F. Bosworth, ambaye wengi wenu mlikuwa ni rafiki yenu, na mlimjua, na huduma yake ilikuwa na manufaa sana kwangu kama mhudumu kijana. Nilianza mikutano yangu, nami nikakutana na Ndugu Bosworth. Yeye alikuwa na mazoea ya kusema, "Uponyaji wa Kiungu," ni tamshi dogo lisilo zuri sana sasa, yeye alisema, "Uponyaji wa Kiungu ni chambo katika ndoana ya samaki." Kasema, "Kamwe humwonyeshi samaki ndoana. Unamwonyesha chambo, na ndipo anakiendea kile chambo na kushikwa na ndoana." Kwa hiyo hilo ndilo tunalojaribu kufanya. Hilo ni ninii yetu . . . sisi . . . Lengo letu ni kuwaleta watu kwa Bwana Yesu Kristo. Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kwa hiyo kama Yeye alikuwa ni Mponyaji katika siku zilizopita, Yeye ni Mponyaji leo.

30 Ushuhuda tu wa kibinafsi kabla sijawaombea wagonjwa wanaosikiliza redio. Ilikuwa ni siku chache zilizopita, nilikuwa nimeketi huko juu milimani ambako jambo kubwa lilikuwa limetukia mbele ya ndugu kumi na watano ama ishirini kule, ambako Malaika wa Bwana alishuka chini jinsi hiyo, na Nuru kuu ikiruka kama kimondo ikilipuka, na ipenye kila mahali, kwa ghafla milimani, na miamba ikirushwa umbali wa futi mia mbili, ama zaidi, kote ardhini, ikikata vilele vya miti. Nami nilikuwa nimesimama papo hapo chini Yake. Na niliwaambia dakika chache tu kabla halijatukia, kwamba jambo hilo lingetukia na yale ambayo yangetukia; kwa kweli, ilisemwa jana yake. Na watu hawa wote wakikimbia chini ya malori na cho chote kile,

wakijaribu kutoroka. Hawakujua kilichokwisha tukia. Naye alinena na kusema mambo ambayo yangetukia papo hapo mara baadaye.

31 Nikiketi kwenye mwamba fulani huu pale, mahali pale hasa Yeye alipokuwa ametokea, nilikuwa na ra—rafiki aliyekuwa pamoja nasi, aliyekuwa ameshuka kuja kutoka Minnesota. Watu wake wako hapa asubuhi ya leo na sina hakika ila huenda yeye yuko hapa kwenye baadhi ya orafa nyingine. Ilikuwa ni Donavon Weerts, pia jamaa mdogo mzuri, Mluteri ambaye ndiyo kwanza ampe Kristo maisha yake na kujazwa na Roho. Mvulana mnyenyekevu sana wa Kijerumani, ana umri upatao miaka thelathini, familia, watoto wawili watatu wadogo. Alihamia Tucson apate kuwa tu jirani yangu, ambapo watu mia tatu ama mia nne walikuwa wamehamia kule wapate kuwa majirani. Kwa hiyo yeye . . .

32 Nami ninafurahia kuwa na majirani kama hao. Wananifuata mpaka Afrika Kusini, na kila mahali, wapate tu kuwa karibu na kuona . . . pamoja nami, na kuwa pamoja nami na kufurahia raha za Bwana.

Jamaa mnyenyekevu sana, sikuwa nimemfahamu sana.

33 Bila shaka, watu ninaojua na ninaoshirikiana nao ni kama ndugu yangu wa kuzaliwa tu, dada yangu. Ninawaangalia, na ninajisikia ya kwamba kama wanaenda isivyo, nami huwachukua kando na kuzungumza nao, kwa maana ninawapenda. Tunataka kuishi Utukufuni pamoja. Na mara kwa mara labda, mikutanoni, mnafikiri ninawazungumzia kwa ukali. Sivyo ilivyo. Hiyo si kwa sababu kwamba siwapendi, lakini linatoka moyoni mwangu, kwa sababu mi—mimi . . . Halina budi kuwa ni njia moja tu. Kuna njia moja tu ya kumtumikia Mungu, na hiyo ni . . . Nasi hatuna budi kusimama katika njia Yake, haidhuru mawazo yetu yakoje. Njia Yake!

34 Na nilimwona Donavon, kwenye ncha ya kulia ya sikio lake, lilikuwa limevimba kufikia labda mara tatu ya ukubwa wake, na lilionekana jekundu sana. Vema, sasa nikifikiri labda kwa kuwa tumekuwa tuko huko nyikani kwa siku chache, ya kwamba mahali tulipokuwa, ya kwamba labda alikuwa amechomwa sikioni na mpungate. Lakini, nilipokuwa ninaushika mkono wake, niliona ya kwamba ilikuwa ni kansa. Kwa hiyo nikamwambia Donavon, nikasema, “Donovan, je! wewe umeninii . . . Hiyo imekuwa kwenye sikio lako kwa muda gani?” Kumtania tu kwa namna fulani, kana kwamba sikujua. Nikasema, “Hiyo imekuwa kwenye sikio lako kwa muda gani, Donavon?”

Akasema, “Ndugu Branham, yapata miezi sita,” alisema.

Nikasema, “Kwa nini hukunigusia jambo hilo?”

35 Akasema, “Loo, ni kuona wewe una shughuli nyingi,” kasema, “Sikutaka ku—kufanya jambo hilo.” Kasema,

"Niliwazia tu labda wakati mwingine huenda Bwana akakwambia."

Kwa hiyo nikasema, "Je! Unatambua ni kitu gani?"

Akasema, "Nina fununu ya hakika."

Nikasema, "Hiyo ni kweli."

36 Na asubuhi ya pili. Si kufanya zaidi ya hayo, kumshika mvulana huyo kwa mkono; asubuhi yake, hakukuwako hata na sugu kwenye sikio lake. Ilikuwa imeondoka kabisa.

37 Mara nyingi sana tunashinikiza, tukikazana kufikia *hiki, kile*. Ama . . . Unaona, ni, "Ishara hizi zitafuatana na mwamini." Halikusema "kama wangewaombea wagonjwa." "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya!" Hatuna budi kuwa na imani, sisi wenyewe, katika yale tunayofanya. Vema.

38 Kwa hiyo sasa labda Donavon yuko hapa. Mtakutana naye. Atakuwa hapa, endapo hayuko hapa asubuhi ya leo, kwenye moja ya orofa hizi nyingine. Mtakutana naye, naye atajua ushuhuda huo.

39 Basi ningeweza kusema nini zaidi? Ninaamini Luka, ama Yohana, mmoja wao, alisema ulimwengu usinge-. . . kutoshikilia, tosha kwa vile vitabu vingeweza kuandikwa juu ya yale aliyoyatenda miongoni mwa watu katika siku hizi za mwisho; jinsi wagonjwa walivyoponywa, walevi sugu wamekombolewa, kwa maelfu yao, na kila namna ya magonjwa na mateso.

40 Sasa, ninyi mnaosikiliza redio huko nje, pamoja na hapa, ninashikilia hapa sasa kiganja kilichojaa tele mahitaji yaliyotumwa kwa simu asubuhi ya leo, imekuwa ikiita daima tangu tulipokuja hapa. Na kwa hiyo sisi . . . Maombi mia moja na tisini na sita yamekuja asubuhi ya leo, kwa simu, tangu tulipokuja hapa. Kwa hiyo hebu na tuungane katika maombi sasa wakati kila mmoja . . . Po pote mlipo, huko nje nchini, wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, kama ninyi ni waamini. Kama si waamini, wekea mkono juu ya Biblia ama kitu fulani huko nje, tunapoomba kwa ajili ya hapa na huko.

41 Baba mpenzi wa Mbinguni, huo ushuhuda mdogo wa Donovan Weerts, mmoja tu wa maelfu, Bwana, ambao Wewe kwa neema sana . . . Ninaomba ya kwamba utaangalia chini kwenye mioyo ya watu walio hapa na wanaosikiliza kwa njia ya redio. Naomba pia uwajalie, kila mmoja wao, aponywe. Naomba yule mwovu awaache, na jalia wakombolewe na mateso yao yote. Tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao, tunaomba. Amina. "*Asante, Bwana* . . ." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

[Ndugu Branham anamaliza matangazo ya pili ya redio—Mh.]

☆ ☆ ☆ ☆ ☆ ☆ ☆

42 Vema, hii ni mara ya tatu ya mimi kuwa hapa asubuhi ya leo. Jamani! Na, mnajua, tuliambiwa sasa hivi ya kwamba inatupasa kuondoka humu jengoni katika dakika kumi na mbili hivi, kumi na nne, ama kitu kama hicho. Na menejimenti walisema, ambao wako huko kwenye orofa hiyo nyingine, nao hawawezi kuandaa chakula cho chote. Mlo wetu ulikuwa mrefu. Sisi tuna awamu nyingi za mlo, mnajua. Kwa hiyo tuna furaha sana, sana ya kwamba tumekuwa na jubilii hii kuu ya mlo wa kiroho, kama ambavyo ningeliliita jambo hili, asubuhi ya leo hapa pamoja na kundi hili zuri la watu.

43 Ningetaka ku—kutaja ya kwamba tunaninii . . . huduma tena, kesho alasiri, huko kwenye Embassy. Sasa, tutakuwa tukiwaombea wagonjwa kule, na kumtarajia Mungu kukutana nasi. Nami nimekuja kutimiza sehemu yangu, huduma yangu, katika kufanya (yote tuwezayo) kuufanikisha mkutano huu. Si kufanikiwa kwa sababu ni mikutano yetu, bali ni kufanikiwa kwa watu kumpata Yesu Kristo. Hayo ndiyo mafanikio. Mikutano yo yote, haidhuru tunamsifu Mungu jinsi gani, kwamba ni mambo mangapi makuu tunayomwona akifanya, kwamba ni mara ngapi Yeye ananena nasi katika Roho, na kadhalika; mpaka kuwe kuna jambo fulani limetimizwa, watu zaidi waingizwe katika Ufalme!

44 Na Ndugu Shakarian sasa ndio kwanza atoe ta—tamshi la kweli sasa hivi juu ya vile anavyofikiria juu ya siku hizi tu—tunazoishi. Kwa kweli ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote, ya kwamba tunaishi kabisa kwenye mwisho wa wakati, katika ninii tu—katika tu vivuli vya jioni. Jua limeenda sana. Na tunapoona mambo yakitokea jinsi yalivyo leo, mbona, ni vigumu kusema yale kizazi kingine kingeleta. Siku chache zilizopita . . .

45 Hebu acheni niwape jambo fulani la kina kidogo. Walifanya utafiti Arizona kote, ambako ninaishi, wa shule zote. Waliwapa watoto, bila ya wao kujua, chemsha bongo. Na unajua nini? Pamoja na shule za sekondari ya juu na—na za sekondari ya taaluma, kulikuwako na asilimia themanini ya watoto waliougua upungufu wa akili. Asilimia sabini yao walikuwa ni wenye kuangalia televisheni. Unaona, hayo maovu, yamepenyeza tu kwetu nasi hatuninii . . . Unashangaa ni kwa nini jambo hilo linatokea. Mnaweza kusikia sauti ya Mungu ikipiga makelele dhidi yake, na hata hivyo hapa tuna—tunajikuta tumezingirwa ndani yake.

46 Hebu niwape jambo fulani la kushtusha. Unaona, "Si wote wanaoniambia Mimi, 'Bwana, Bwana,' watakaoingia; bali ni yule afanyae mapenzi ya Baba Yangu." Mapenzi Yake ni Neno Lake. Tunaweza kuwa wa kidini sana, tuwe na wakati mzuri sana, kupaza sauti, kuruka, katika mikutano hii, ambayo tunaninii . . . Sitaki—sitaki kuwa mkosoaji. Bali nina wa—wajibu kwa Mungu, na wajibu huo ni kuwa mwaminifu na kusema yale anayonitaka niseme. Nami kwa kweli nina—ninashukuru kwa ajili ya tawi

hili la California ambao wamenivumilia katika—katika imani yangu. Kama sishuhudii imani yangu, mimi ni mnafiki na sasa hata si mwaminifu kwenu. Na kama siwezi kuwa mwaminifu kwenu, nitakuwaje mwaminifu kwa Mungu, maana ninawaona na kuongea nanyi. Bila shaka, tunafanya hivyo, kwa Mungu, pia, bali hatuna budi kuwa waaminifu kabisa na wakweli mmoja kwa mwingine. Bila shaka tuko katika kipindi ki—kibaya, kibaya sana. Na hivi uliwahi kutulia . . .

47 Hebu tu niwape uchambuzi mdogo. "Si wote waniambiao, 'Bwana, Bwana,' watakaoingia; bali ni yule ayafanyaye mapenzi ya Baba Yangu." Yesu alisema, duniani, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno." Kila Neno! Si tu mara kwa mara, Neno, bali kwa kila Neno.

48 Ilikuwa ni Neno moja lisiloaminiwa, na ninii ya Mungu . . . la amri za Mungu, lililosababisha mauti, huzuni, na kila maradhi na magonjwa ya moyo, kukosa Neno la Mungu, Neno moja! Kama aliipeleka jamii ya mwanadamu mautini, kwa kukosa, kutokuamini Neno moja, "hakika," hakika. Bali Yeye alisema lingetukia. Shetani akasema, "Hakika halitatukia." Lakini lilitukia.

49 Kwa hiyo, inatupasa kutimiza kila Neno la Mungu. Na kama mwanadamu na kuteseka huku kote na kadhalika kulikoingia kwenye jamii ya mwanadamu, kwa kuelewa vibaya, ama—ama kutokuamini Neno moja, tutarudi namna gani kwa kuacha Moja, kama liligharimu gharama hii yote, hata uhai wa Mwanawe?

*. . . wengi wanaitwa, . . . wachache wanachaguliwa.*

*. . . wengi wanaitwa, . . . wachache wanachaguliwa.*

50 Siwezi kuchukua somo kutoka kwenye jambo hili, bali sababu hatuna wakati, lakini ili tu kuwaachia jambo fulani. Hebu na tufikirie juu ya . . .

51 Nilienda siku moja pamoja na Ndugu Shakarian, mahali walipokuwa wakiwazalisha ng'ombe. Nami nikaona ninii—ninii . . . katika maabara ambako Ndugu Shakarian alinipeleka. Nao wakatumbukiza kwenye mbegu za dume la ng'ombe, kidogo tu . . . kama chombo kidogo, mti wa kiberiti, na kuchukua lundo la mbegu hiyo, na kuliweka chini ya darubini hii iliyoikuza mara mia kadha. Na kulikuwako na seli zazi zikirukaruka ndani yake, katika mbegu hizo za dume. Ambapo, tunajua seli zazi hutokana na dume, na yai kutoka kwa jike. Nami nilimwuliza mkemia kule, nikasema, "Ni vitu gani vile vidogovidogo vinavyorukaruka namna hiyo?"

Akasema, "Hao—hao ni fahali wadogo na ndama wadogo." Unaona?

Ndipo nikasema, "Kwenye tone hilo dogo?"

Akasema, "Ndiyo."

52 Nikasema, "Labda basi kwenye mbegu zote kungekuwako na milioni moja ya hizo?"

Akasema, "Loo, naam." Unaona? Sasa, angalia kwa makini.

53 Sasa, wakati jambo hili kuu linapotukia, kuna yai moja linalongojea seli zazi moja kutoka katika milioni hiyo. Wala hakuna mtu anayeweza kujua ni seli zazi ipi hiyo, ama ni yai lipi hilo. Kama ungeangalia uzazi wa kawaida, ni mwujiza mkubwa kuliko ninii—kuliko uzazi wa kibikira. Kwa sababu, katika mbegu hizi za kiume, kuna moja mle ndani iliyochaguliwa tangu zamani kuishi, na hizo nyingine zitakufa. Wala si ile ya kwanza inayokutana; ni ya kwanza inayokutana na yai. Labda yai litainuka kutoka upande wa nyuma wa hizo mbegu za dume, ama katikati ya hizo mbegu za dume; seli zazi inaweza kufanya vivyo hivyo, yai. Seli hiyo zazi inatambaa kuingia kwenye hilo yai, na mikia midogo inakatika na kuanguka, na hapo uti wa mgongo unaanza. Kuna moja tu katika lundo hilo lote, la milioni moja, itakayofaulu, moja tu; na hiyo inaamuliwa na Nguvu fulani isiyojulikana, kwa mwanadamu. Hata hivyo mnaninii, kila moja, inafanana na nyingine, kila moja ya hizo seli zazi zinafanana kabisa. Ni jambo lile lile katika wanyama. Ni jambo lile lile katika mwanadamu. Inaamuliwa kama itakuwa ni mvulana, msichana, mwenye nywele nyekundu, nyeusi, ama cho chote kile. Inaamuliwa na Mungu. Zote zinafanana, kimaumbile, bali kuna moja mle ndani ambayo imekusudiwa uzima; moja katika milioni moja, hata hivyo zote zinafanana.

54 Wakati Israeli walipoondoka Misri, kulikuwako na karibuni watu milioni mbili walioondoka wakati huo huo. Kila mmoja wao alisikia ujumbe wa nabii. Kila mmoja wao aliona ile Nguzo ya Moto. Kila mmoja wao alibatizwa katika Musa, katika Bahari ya Shamu. Kila mmoja wao alipaza sauti katika—katika Roho, wakapiga tari na kukimbia huku na huko kwenye ukingo, pamoja na Miriamu, wakati Musa alipoimba katika Roho. Hao, kila mmoja wao, aliunywea Mwamba ule ule wa kiroho. Hao, kila mmoja wao, alikula Mana mpya kila usiku. Kila mmoja wao! Bali kulikuwako na wawili waliofaulu kuingia kwenye ile nchi, mmoja katika milioni moja.

55 Jaribio lilikuwa ni nini? Wote walinywea Mwamba ule ule, wote walikula Mana ile ile ya kiroho kama tunavyokula asubuhi ya leo, bali jaribio la Neno liliwaonyesha walivyo. Hapo ilipofikia wakati wa Kadeshi-barnea, wakati walipoanza kuingia kwenye ile nchi ya ahadi, nao wasingeweza kuingia mpaka walipojaribiwa kwa Neno. Na wote hao ninii—wengine kumi walirudi, na kusema, "Hatuwezi kufaulu! Watu hao ni kama. . .Sisi ni kama panzi, kwao, miji yao mikuu iliyozungushiwa kuta. Upinzani ni mkubwa mno."

56 Bali Yoshua na Kalebu wakawatuliza watu. Wakasema, "Sisi twaweza hata na zaidi kulifanya jambo hilo!" Kwa nini? Mungu

alisema, kabla hawajaondoka kwenye nchi ya ahadi, "Nimewapa ninyi hiyo nchi. Nimewapa ninyi. Ni yenu." Lakini kulikuwa na mmoja kutoka katika kila milioni moja.

57 Kuna karibu watu milioni mia tano wanaojiita Wakristo ulimwenguni leo, na kila siku inamalizia kizazi. Na sasa, vipi kama Unyakuo ungetokea leo na watu mia tano, kote ulimwenguni, wangechukuliwa katika Unyakuo huo? Hamngejua kamwe wala hata kuliona gazetini, habari ya kuondoka kwao. Na kule Kuja kwa Bwana ni Kuja kwa siri. Yeye atakuja anyakue na kutoweka. Itakuwa ni wachache sana, hata . . .

58 Kama tu ilivyokuwa katika siku ambazo wanafunzi walimwuliza Yesu, "Kwa nini Waandishi wanasema ya kwamba—ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?"

Akasema, "Yeye amekuja tayari, wala hamkujua jambo hilo."

59 Je! uliwahi kuwazia kile watu walichofanya? Waliendelea moja kwa moja kuamini ya kwamba Mu-. . .ya kwamba Eliya alikuwa anakuja. Naye alikuwa papo hapo miongoni mwao, wala hawakujua hilo.

60 Ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu! Watamfanyia jambo lile lile. Roho wa Mungu yuko hapa. Vema, tutafanya nini Naye? Je! tutakula Mana, na kadhalika, wala tusiendelee kusonga mbele tunapokua?

61 Je! ulipata kuona mbegu fulani, kama vile Kasisi Pitts alivyokuwa akinena muda mchache uliopita, na jinsi mbegu inavyoingia ardhini? Mbegu nyingi zimo ardhini. Wakati Mungu alipotulia juu ya maji, pamoja na Nuru, nayo Nuru ikaleta. Uwepo wa kwanza wa Mungu, Nuru iliyonenwa ilikuja kwa Neno la Mungu. Na Neno la Mungu ndilo tu jambo pekee ambalo lingali linaleta Nuru. Na wakati maji yaliponywea, ile mbegu tayari ilikuwa ardhini, na hiyo Nuru ilichipuza tu mbegu zilizokuwa zina seli zazi ndani yao, zikachipuka. Mungu akifanya uumbaji Wake.

62 Na sasa, kwenye asubuhi ya Pasaka kulikuwako na Nuru nyingine iliyokuja duniani, wakati Roho Mtakatifu alipotolewa. Naye anatolewa apate kuleta Nuru kwa hizo Mbegu ambazo Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, alijua kwamba zingekuwa hapa duniani. Kama alivyojua mbegu ya kwanza ya asili, Yeye anajua ambapo Mbegu ya Kiroho ipo. Mwili wako ulikuwa upo hapa wakati uo huo duniani, wakati Mungu alipoumba nchi mara ya kwanza. Sisi ni sehemu ya nchi. Tulikuwa tuko humo. Na kwa kujua Kwake tangu zamani Yeye alijua ni nani hasa angempenda na ni nani angemtumikia, na ni nani asingemtumikia. Kujua Kwake tangu zamani kunaonyesha jambo hilo. Kama hakuonyeshi, basi Yeye si Mungu. Hawezi

kuwa Mungu bila kuwa hana kikomo. Na kama hana kikomo, Yeye anajua mambo yote.

63 Kwa hiyo, unaona watu wakifanya makosa yao ya kijinga. Wanakwazwa nalo. Wanalikimbilia, nao wanawazia *hivi* na *vile*, bali halifanikiwi, tunaliona. Bali kuna kufanikiwa, huko ni kupata mapenzi makamilifu ya Mungu na kuyashindania, kile Mungu alichokuitia.

64 Kama vile Ndugu Jack alivyosema muda mchache uliopita kuhusu hapa chini kwenye—kwenye Persian Square, machafuko yote. Mmoja *hivi*, na mwingine *vile*; na kuhusu wanatheolojia, na kadhalika, kwamba unataka kujua theolojia kidogo, ushuke uende kule.

65 Nafikiri hilo ni kama tu ilivyo katika Bustani ya Hyde huko London. Nilikuwa kule, kila mtu ana wazo lake mwenyewe. Ni—ni mkusanyiko wa ulimwengu wa kisasa katika Babeli.

66 Lakini je! umeona ka—kama vile Ndugu Pitts alivyoendelea na ujumbe wake mzuri asubuhi ya leo kwetu? Wakati alipoanza kutoka kwenye ile bustani, hapo aliona yungiyungi dogo la Pasaka. "Katikati ya mchafuko huo wote," kama alivyotuelezea, "halikuwa na njia ya kusema 'ndiyo' ama 'hapana.' Ilikuwa ni uhai wa Mungu ukiangaza ndani yake, katikati ya mchafuko huo wote." Lilikuwa liko hapo katika uangavu wake, kwa maana Mungu alikuwa ameliamuru liwepo hapo. Katikati ya mkwaruzano wote, hakuna mtu aliyekuwa akiliona. Hawakuona maana yake kiroho.

67 Na ndivyo ilivyo leo miongoni mwa makusanyiko yetu yote makuu na makundi, na makanisa na madhehebu, na kadhalika. Moja linavuta *hivi*, "Hatuna budi kuwa Wabaptisti, ama kuwa Wapresbiteri, hatuna budi kuwa *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*." Katikati ya hayo yote, kuna ua linalokua. Kuna nguvu za Mungu papa hapa miongoni mwetu, zinazojikusanya katikati yetu sisi sote. Hebu na tusimame na kuliangalia hilo, dakika chache, na kuliangalia juma hili, na tulione likijifunua papa hapa mbele yetu. Tunaamini ya kwamba Mungu atafanya jambo hilo. Mnalionaje? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

68 Ninaona ya kwamba inatupasa kuwa tumekwisha kushuka kule chini wakati huu. Kwa hiyo na tuombe, kila mmoja wetu.

69 Mungu mpenzi, tunapoinamisha vichwa vyetu katika Uwepo Wako, tunajisikia ya kwamba hatustahili kuomba kabisa. Lakini Wewe ulituahidi ya kwamba, kama tungekuja, hungetukatalia. Na matamshi haya makali ambayo ndiyo kwanza yatolewe, yasiwe fundisho kwa vyo vyote vile, "mmoja katika milioni moja," bali kwa namna tu ya kukumbuka. Kwa maana Wewe ulisema:

> . . .*mlango ni mwembamba, na njia imesonga*, ile *iendayo uzimani, na itakuwa nao* watakaoiona *ni wachache.*

*Kwa maana waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache.*

70 Ee Baba wa Milele, tutumie Nuru ya Injili kote katika jiji hili, katika juma hili lijalo la mkutano. Na endapo kuna Mzao wo wote, kwa namna fulani kwa uteuzi Wako Mwenyewe wa hekima ulio mkuu, kama vile nilivyojaribu kuonyesha jambo hilo katika mbegu za dume na za jike, naomba waingie kwenye mkutano huu. Roho Mtakatifu na awape Nuru. Tunatambua ya kwamba wakati labda umeenda zaidi ya tunavyodhania umeenda. Tunaomba, Mungu, ya kwamba tunapokuja hapa, tukiamini tu ya kwamba labda kuna jambo fulani hapa ambalo lingeweza kutendeka ambalo lingewasaidia watu, ama—ama kumshika yule kondoo wa mwisho. Tunajua, wakati zizi la kondoo litakapojaa, basi Mchungaji atafunga mlango.

71 Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wakati yule mshirika wa mwisho wa familia alipoingizwa, Mungu aliufunga mlango. Nao wakaupiga na kuugonga kwa nguvu, lakini ilikuwa wamechelewa sana. Mungu mpenzi, walipata nafasi.

Wewe ulisema, "Mimi ndiye huo Mlango wa zizi la kondoo."

72 Na ni wa ajabu jinsi gani huo wimbo kutoka kwa mshairi, "Je! tisini na tisa hawakutoshi Wewe? Lakini, la, kulikuwa na mmoja zaidi." Huenda akawa ni maskini kondoo mdogo mweusi, ama huenda akawa ni mtu mdogo ovyo ovyo, huenda akawa ni maskini msichana mdogo ama mvulana mdogo. Hatujui mahali walipo, lakini huyo wa mwisho hana budi kuingia na ndipo mlango utafungwa. Ee Mungu, unayejua mambo yote, yachunguze maisha yetu asubuhi ya leo. Na ututume po pote ambapo kwamba tunaweza kwenda, tuweze kumpata huyo wa mwisho, kusudi mlango ufungwe na Mchungaji awe ndani pamoja na kondoo. Tujalie, Bwana. Kama kuna huyo mmoja hapa leo, kama huyo mmoja anayepaswa kuingia . . .

73 "Wote alionipa Baba Yangu watakuja Kwangu. Wala hakuna mtu awezaye kuja, isipokuwa amevutwa na Baba Yangu."

74 Na endapo kuna mvuto, ama hisia ndogo, ya kwamba huenda hii ikawa ndiyo ile saa kwa ajili ya mtu fulani hapa katika wasikilizaji hawa, hapa ama kule chini, ama po pote wanapoweza kuwa, jalia wajibu, "Naam, Bwana, mimi ni maskini mtu huyo anayetangatanga ambaye ametanga mbali; na ambaye nimelipiga vita jambo Hilo, maishani mwangu mwote. Ni—ni—nilijisikia ya kwamba inanipasa kuja, bali leo ninaning'inia upande wa kushindwa. Siwezi kupanda wala kushuka. Siwezi kupitia njia yo yote." Loo, jalia yule Mchungaji mkuu aje, anyoshe chini mikono ya upendo na kumwingiza huyo mmoja salama, amweke mabegani Mwake na kumrudisha salama.

75 Labda kuna mmoja hapa, Bwana, aliye mgonjwa, katika hali hiyo hiyo, ambaye daktari alisema, "Hakuna la kufanya."

Alijaribu sana kumwokoa, bali asingeweza kumwokoa. Hawezi kumfikia kamwe. Hakuna—hakuna jambo analoweza kufanya. Madawa yake ama kisu chake haviwezi kumfikia. Lakini, Ee Bwana, hakuna kitu kilicho mbali sana kwa mkono Wako mkuu, na Neno Lako ndio mkono Wako. Kwa hiyo tunaomba, Mungu mpenzi, ya kwamba, asubuhi ya leo, wakati tunapozungumza Nawe, ya kwamba wewe utaunyosha mkono Wako chini na kumgusa huyo aliye mgonjwa wala hawezi kujisaidia, asiyeweza kufikiwa na mambo yote ya kisayansi, aliye mbali na daktari, jalia waponywe. Tujalie, Bwana.

76 Tunapowazia habari za Daudi, wakati alipopewa jukumu juu ya kondoo wachache, wachache tu. Lakini siku moja dubu alikuja akamkamata huyo kondoo mmoja mdogo na akamtoa nje, na angalimla (kama vile kansa ingeula mwili fulani), ama simba mkubwa sana. Lakini Daudi, akiwa hajajiandaa vizuri kwa bu—bunduki, ama, akiwa si hodari wa kutumia upanga, bali akiwa tu na kombeo, alimfuata huyo kondoo. Na wakati alipompata m—mnyama aliyekuwa karibu kumwua maskini kondoo huyo mdogo, akamwua kwa kombeo. Silaha rahisi tu ya ngozi na kamba, na, lakini yeye alikuwa anaiamini.

77 Hatuna watu wenye kipaji asilia miongoni mwetu, Bwana. Sisi ni watu wa kawaida walio na maombi machache manyofu, bali tunamfuatilia kondoo wa Baba yetu asubuhi ya leo. Mwanamke yule ambaye amezurura mitaani, kwa huzuni, akivuta sigara, akijaribu kupata amani kwa sigara; mwanamume yule ambaye amenusa bilauri na akajaribu kuirudisha, lakini adui anamshikilia kwa nguvu; huyo mvulana ama msichana ambaye amejaribu kufanya yaliyo sahihi, ambaye hawezi tu kupata nguvu za kuacha mambo mabaya; tunakuja katika Jina la Bwana Yesu, kumdai kondoo huyo asubuhi ya leo. Tunamkataa adui katakata; kwa sababu ni kitu rahisi, kombeo, sala, lakini tunakuja kumrudisha huyo kwenye zizi la Baba yetu, tupate kutoa hesabu ya mambo hayo ambayo tumekabidhiwa mkononi mwetu. Jalia nguvu za Mungu sasa ziiguse imani, ndani ya mioyo ya watu, na jalia mtu huyo aliyepotea arudi asubuhi ya leo. Jalia majaribu ya maisha haya yawageuze, yamwaachilie. Na jalia ajikute salama kwenye mabega ya Bwana wake, akirudishwa kwenye usalama tena. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

78 Mungu awabariki nyote. Mpaka nitakapowaona kesho, nitairudisha ibada kwa Ndugu Shakarian. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

[Ndugu Branham anamalizia sehemu ya tatu—Mh.]

☆ ☆ ☆ ☆ ☆ ☆ ☆

79 Hii, na—natumaini ya kwamba mtaninii. . .ya kwamba nimepata neema zaidi machoni pa Mungu na mbele zenu, kuamini ya kwamba ningesimama hapa kuwaambia jambo

ambalo ni kosa. Nimepita siku yangu ya hamsini na sita ya kuzaliwa kwangu, hivi majuzi. Huu si Ujumbe tu wa mzee. Nimeuamini huu tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Na kama hii si kweli, nimekuwa mtu mpumbavu sana ambaye Mungu alipata kuwa naye duniani. Nimeyatoa maisha yangu yote kwa Imani hii. Na hebu niseme jambo hili kwa uaminifu: kama ningalikuwa na miaka ya kuishi elfu kumi, nisingelibadili maoni yangu.

80 Sasa, kila mtu anaweza kuponywa. Kumbuka, uponyaji umo ndani yako. Mungu aliweka kwenye mpichi kila tunda la pichi litakalozaliwa ndani yake, wakati alipoupanda katika ile Bustani. Unaona, unaninii tu. . . mpichi ama mtofaa, ama mti wa matunda, unapaswa tu kukua, kutokana na kunywa maji ya ardhini. Sasa kila mmoja wenu ana nguvu hizo zikilala ndani yenu, za kuwakomboa, kwa kuwa ni Mungu, kwa sababu mmepandwa katika Kristo kwa ubatizo (si ubatizo wa maji), ubatizo wa kiroho. Huji katika Kristo kwa ubatizo wa maji. Ni kwa ubatizo wa kiroho!

81 Kesho alasiri, Bwana akipenda, ninazungumzia juu ya jambo hilo, kwamba matumizi Yake ni *yapi* na ni ya *namna gani*. Tunaufanya alasiri kwa hiyo hautaingiliana na ibada zenu zo zote.

82 Sasa angalia, kila mmoja wenu hapa anasimama kama waamini, unaona, ndipo Uzima uliokuwamo ndani ya Kristo umo ndani yenu. Huo unaweza, kama ungeweza tu kuona jambo hilo!

83 Ni kazi ya Ibilisi kuwakinga msione jambo Hilo, kuwafanya vipofu. Anaweza tu kuwaacha mpofushwe, hiyo ni kusema, unaona, hujui mahali unakoenda basi. Mtu aliye kipofu hawezi kujua mahali anakoenda, inambidi kutafuta ujuzi kutoka kwa mtu anayeweza kuona. Mpaka tutakapoweza kufahamu, itambidi mtu fulani kutwambia kwamba Kweli ni nini.

84 Na Kristo alikufa kwa ajili yako, nawe unahamishwa kutoka ulimwenguni na kupandwa katika Kristo. Na kila unachohitaji kimo moja kwa moja ndani yako, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo si ni kweli? Sasa jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuanza tu kunywa kutoka Kwake.

85 Na mti unapokunywa, unaanza kutoa majani yake, chipukizi lake, unatoa tunda lake kila mwaka. Tunda hilo halimo ardhini; tunda hilo limo ndani ya mmea huo. Ni wangapi wanaofahamu jambo hilo, semeni "amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa hiyo, unaona, tunda hilo limo kwenye mmea, na kila mmea hauna budi kunywa kutoka kwenye chemchemi yake. Wakati mvua inaponyesha, inaupa mmea huo, uhai, wa kuunywa. Na, hapo unapokunywa, unakua.

86 Na unakua mpaka unafikia kwenye chipukizi kamili, kama vile tu Kanisa lilivyofanya, lipate kustawi katika wakati huu.

87 Na, tunapokunywa, tunakua. Bali kama mmea ukikataa kunywa, basi mmea huo hauwezi kukua. Na laiti tu utaliamini jambo hilo sasa, kibinafsi!

88 Bila shaka, unajua jinsi Bwana anavyofanya jambo hilo, anavyoonyesha mambo mbalimbali, ya yale uliyofanya na yale hukupaswa kufanya, na kadhalika, mkutanoni. Tulikuwa tukitarajia ya kwamba Roho Mtakatifu angetushukia asubuhi ya leo na kufanya mambo hayo, tulipokuwa tumesimama. Lakini niliendelea kungojea.

89 Nafikiri ni kwa ajili ya kuwa na wasiwasi, nikifikiri ya kwamba huko chini wanatutaka tutoke humu, unaona. Lakini wanatutaka; tumechelewa sasa.

90 Lakini aminini jambo hili, kwa moyo wenu wote. Tafadhali aminini. Iwapo mimi—iwapo nimepata neema mbele zenu, kama mtu mwaminifu, aminini jambo hili. Sasa wekeaneni mikono yenu juu—mmoja juu ya mwingine.

91 Sasa angalieni, sasa, Biblia haikusema, "Ishara hizi zitafuatana na William Branham." Haikusema, "Zitafuatana na Oral Roberts peke yake." Haikusema, "Zitafuatana na Ndugu Kopp," ama mtu fulani.

92 "Ishara hizi zitafuatana na hao," wingi, "waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Ni zile Nguvu za Mungu zilizo ndani yenu, ambazo zinaleta uzima ndani ya mtu huyo unayemwekea mkono, chemchemi iletayo Uzima ya Roho Mtakatifu.

93 Mungu mpenzi, katika Jina la Yesu Kristo, katika wakati huu ulio muhimu sana ambapo kanisa...jalia wasimame kwenye sekunde hii, bila wasiwasi, na jalia Nguvu zilizomfufua Kristo kutoka kaburini, ziwahuishie sasa hivi Ukweli wa Injili, kwamba agizo la Yesu lilikuwa, kama "wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Jalia kila nguvu za pepo, kila maradhi, kila ugonjwa, kila mateso, kila kitu kinachosababisha maumivu kilichotukia kwa watu, naomba kiondoke sasa hivi kwa imani. Kama watu wanaoamini, tunaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

94 Sasa inueni mikono yenu na mumpe sifa, kama mnaamini ya kwamba Yeye anafanya jambo hilo.

95 Mungu mpenzi, mtoto huyu mchanga atakufa, Bwana, isipokuwa jambo hili litendeke. Ninalaani kifundo hiki, katika Jina la Yesu Kristo. Naomba kimwondoke mtoto huyu asiye na hatia. Amina.

Sasa, madaktari wamejaribu, nao wanashindwa. Amini tu.

*Mmoja Katika Milioni Moja* SWA65-0424
(One In A Million)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 24 Aprili, 1965, katika Clifton's Cafeteria kule Los Angeles, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2007 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org